

Maji kama njia ya maisha

Royal Life Saving, tunataka kila Mwaustralia, bila kujali umri wake, uzoefu wake na asili yake kufurahia maji kama njia ya maisha. Hii inamaanisha kwenda nje na kutumia vyema maji, lakini sisi tunahitaji kufanya hivyo kwa njia yenye usalama. Bila kujali umri au uwezo wako, kuna fursa nyingi za kujifunza jinsi ya kuogelea pamoja na kuboresha ujuzi wako wa usalama wa maji.

Tumejumuisha vidokezo kadhaa vya rahisi ili kuhakikisha wewe pamoja na wapendwa wako mnakaa salama ndani na karibu na maji.



Ili kujifunza zaidi kuhusu kuogolea pamoja na jinsi unavyoweza kukaa salama karibu na maji tembelea: drowningprevention.org.au/culturalwatersafety

Kufurahia maji ni njia ya maisha ya Australia...
maji kama njia ya maisha



Tutunzane salama tukiwa karibu na maji



ROYAL LIFE SAVING
NSW | ACT | TAS

Jua mipaka yako na epuka hatari

Kujihatarisha karibu na maji kunaendelea kuwa sababu kubwa ya vifo vya kuzama majini, hasa kwa wanaume wenye umri wa zaidi ya miaka 18.

- Epuka kunywa pombe kabla ya kuingia majini, au wakati unapowasimamia watoto.
- Epuka kuingia majini katika maeneo na hali usizozafahamu.
- Epuka kwenda peke yako. Sio usalama tu, ila ni njia ya kufurahisha zaidi.



Angalia hali ya maji kabla ya kwenda kwenye maji

Mabadiliko ya hali ya hewa pamoja na maji yanaweza kuwa hatari sana.

- Angalia hali ya hewa mtandaoni au kwenye programu ya hali ya hewa na unapofika angalia vizuri hali kabla ya kuingia kwenye maji.



Vaa koti la kuokoa maisha wakati unapokuwa kwenye maji

Kila mtu, hata waogeleaji wenye uzoefu, wanapaswa kuvaa koti la kuokoa maisha wakati wakiwa kwenye maji, kwani huenda ukahitaji kukaa muda mrefu kwenye maji ikiwa ajali itatokea.

- Vaa koti la kuokoa wakati ukiwa kwenye mashua, wanaoendesha kwenye jet ski, kusafiri kwa tanga, kupanda mtumbwi, kukayaki, kupanda kasia na uvuvi kutoka kwenye miamba hadi baharini.

Wasimamie watoto wako kila wakati

Usimamizi ndio jambo muhimu zaidi unaweza kufanya ili kuwaweka watoto wako salama wanapokuwa karibu na maji. Kumbuka, usumbufu wowote ni hatari na huwaweka watoto wadogo katika hatari. Hatua hizi za kuzuia kuzama za Keep Watch zitakusaidia wewe kuwaweka watoto wako salama wanapokuwa karibu na maji.

- **Simamia.** Simamia watoto kikamilifu wanapokuwa karibu na maji.
- **Zuia.** Zuia ufikiaji wa maji kwa watoto.
- **Fundisha.** Wafundishe watoto ujuzi wa usalama wa maji.
- **Itikia.** Jifunze jinsi ya kukabiliana katika kesi ya dharura.

